

## **Swahili A: literature – Standard level – Paper 2**

### **Swahili A : littérature – Niveau moyen – Épreuve 2**

### **Swahili A: literatura – Nivel medio – Prueba 2**

Thursday 11 May 2017 (morning)

Jeudi 11 mai 2017 (matin)

Jueves 11 de mayo de 2017 (mañana)

1 hour 30 minutes / 1 heure 30 minutes / 1 hora 30 minutos

---

#### **Instructions to candidates**

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Answer one essay question only. You must base your answer on at least two of the part 3 works you have studied and compare and contrast these works in response to the question. Answers which are not based on a discussion of at least two part 3 works will not score high marks.
- You are not permitted to bring copies of the works you have studied into the examination room.
- The maximum mark for this examination paper is **[25 marks]**.

#### **Instructions destinées aux candidats**

- N'ouvrez pas cette épreuve avant d'y être autorisé(e).
- Traitez un seul sujet de composition. En basant votre réponse sur au moins deux des œuvres de la troisième partie que vous avez étudiées, vous devez comparer et opposer ces œuvres dans le cadre du sujet. Les réponses qui ne sont pas basées sur au moins deux des œuvres de la troisième partie n'obtiendront pas une note élevée.
- Vous n'êtes pas autorisé(e) à apporter des exemplaires des œuvres que vous avez étudiées dans la salle d'examen.
- Le nombre maximum de points pour cette épreuve d'examen est de **[25 points]**.

#### **Instrucciones para los alumnos**

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Conteste una sola pregunta de redacción. Base su respuesta en al menos dos de las obras estudiadas de la parte 3, comparándolas y contrastándolas en relación con la pregunta. Las respuestas que no se basen en al menos dos obras de la parte 3 no recibirán una puntuación alta.
- No está permitido traer copias de las obras estudiadas a la sala de examen.
- La puntuación máxima para esta prueba de examen es **[25 puntos]**.

Jibu swali **moja** tu la insha. Jibu lako lazima liegemee kwenye **angalau** kazi **mbili** za Sehemu ya 3 ulizojifunza na **ulinganishe na ulinganue** kazi hizi katika kujibu swali. Majibu ambayo hayajadili angalau kazi mbili za Sehemu ya 3 **hayatatzwa** alama za juu.

### Tamthilia

1. Linganisha na ulinganue mbinu zilizotumika kuwasilisha kukua na kubadilika kwa mhusika mkuu katika tamthilia nzima kutoka kwa angalau wandishi wawili wa tamthilia ulizosoma.
2. Linganisha njia ambazo waandishi wa michezo ya kuigiza wanatumia kuwasilisha sifa hasi za wahusika wakuu katika angalau tamthilia mbili za waandishi tofauti. Jadili kwa ujumla umuhimu wa sifa kama hizo katika tamthilia ulizosoma.
3. Waandishi wa michezo ya kuigiza mara nyingi huongeza mvuto katika michezo yao kwa kutoa zaidi ya hadithi moja. Chunguza ni kwa jinsi gani mbinu hii inavyotumika katika angalau tamthilia mbili ulizosoma.

### Riwaya

4. Riwaya nyingine hutumia sauti moja tu kusimulia hadithi, nyingine hutumia zaidi. Linganisha jinsi sauti ya usimulizi ilivyotumika katika angalau kazi mbili ulizosoma, na athari zake.
5. Ni kwa kiasi gani mwisho wa riwaya hutoa suluhisho? Kwa kurejelea kauli hii, linganisha miisho ya angalau riwaya mbili ulizosoma.
6. Waandishi wakati mwingine hutumia ucheshi kutilia mkazo wazo kuu. Kwa kurejelea angalau kazi mbili ulizosoma, linganisha njia ambazo ucheshi umetumika na athari zake.

### Ushairi

7. Linganisha mbinu zilizotumiwa katika kazi za angalau waandishi wawili ulizosoma kuwasilisha mtazamo fulani wa ulimwengu.
8. Ukiirejelea kwa karibu angalau kazi mbili za washairi tofauti ulizosoma, jadili jinsi uteuzi wa maneno kwa uangalifu unawasaidia washairi hao kuandika ushairi unaogusa hisia za wasomaji.
9. Linganisha na ulinganue jinsi angalau kazi mbili za washairi tofauti ulizosoma zimetumia mandhari fulani na athari zinazotokana nayo.

### Riwaya ya mapenzi

10. Linganisha njia ambazo mgongano wa maslahi baina ya wapenzi unavyodhihirishwa katika angalau kazi mbili ulizosoma, na athari zake katika kazi hizo kwa jumla.
  11. Riwaya za mapenzi mara nyingi hutegemea mabadiliko yasiyotegemewa katika msuko ili kumshirikisha msomaji. Ukrejelea kazi za angalau waandishi wawili ulizosoma, linganisha ni kwa njia gani na kwa athari gani zinafanya hivi.
  12. Waandishi wa riwaya za mapenzi huwasilisha wahusika wao kama mifano ya kuigwa. Jadili uhalali wa madai haya ukrejelea kwa karibu angalau kazi mbili ulizosoma.
-